JAMHURI YA MUUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2020

## ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2020

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020**

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO

DIBAJI……………………………………………………………………………..iv
1.0 UTANGULIZI ........................................................................................... 1
2.0 UCHAMBUZI WA KILA SWALI ............................................................. 2
2.1 SEHEMU A: SUNNAH, HADITHI NA TAWHIID................................ 2
2.1.1 Swali la 1: Sunnah na Hadithi - Kuchagua Jibu Sahihi.......................... 2
2.1.2 Swali la 2: Tawhiid - Kuoanisha ........................................................... 8
2.2 SEHEMU B: TAWHID, TAREKH NA QUR’AN................................. 15
2.2.1 Swali la 3: Tawhiid - Kujibu Kweli au si Kweli ................................. 15
2.2.2 Swali la 4: Tarekh - Kujaza Nafasi Zilizowazi ................................... 21
2.2.3 Swali la 5: Qur’an - Kupanga Nukuu Katika Mpangilio Sahihi .......... 27
2.3 SEHEMU C: FIQH ................................................................................ 30
2.3.1 Swali la 6: Kujibu kwa Ufupi.............................................................. 30
2.3.2 Swali la 7: Insha .................................................................................. 38
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA ................................ 43
4.0 HITIMISHO ............................................................................................ 44
5.0 MAPENDEKEZO ................................................................................... 44
Kiambatisho ................................................................................................. 45

## DIBAJI

Hii ni taarifa hii ya Uchambuzi wa Majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kidato cha Pili (FTNA) 2020 somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Madhumuni ya taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla kuhusu ufaulu wa wanafunzi katika upimaji wa somo hili. Majibu ya wanafunzi katika upimaji ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo waliweza kujifunza kwa usahihi na yale ambayo hawakuweza kujifunza katika kipindi cha miaka miwili ya Elimu ya Sekondari (Kidato cha I na cha II).

Katika taarifa hii, uchambuzi wa kila swali umefanyika kwa kina na changamoto mbalimbali zilizojitokeza kwa wanafunzi katika kujibu maswali zimebainishwa na kufafanuliwa. Uchambuzi huu umebainisha wanafunzi waliopata alama za juu, wastani na za chini katika kila swali na sampuli za majibu ya wanafunzi waliofanya vizuri na wale waliofanya vibaya zimeoneshwa. Aidha, sababu mbalimbali ambazo zilichangia wanafunzi kuweza au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi pia zimebainishwa. Sababu zilizowafanya baadhi ya wanafunzi kuweza kujibu maswali kwa usahihi ni pamoja na kuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mada zilizopimwa na kuelewa msingi wa maswali yaliyoulizwa. Aidha, uchambuzi huu umebaini kuwa baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu maswali kwa usahihi hawakuwa na ujuzi wa kutosha katika mada mbalimbali za Elimu ya Dini ya Kiislamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya maswali.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hatimaye kuondoa changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Endapo mapendekezo yaliyotolewa mwishoni mwa taarifa hii yatafanyiwa kazi, kiwango cha kufaulu katika somo hili kinaweza kuongezeka. Baraza la Mitihani linatoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika uandishi wa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imetokana na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kidato cha Pili (FTNA) uliofanyika mwezi Novemba mwaka 2020 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Upimaji huu uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo husika uliotolewa mwaka 2012 kwa Kidato cha I na II.

Karatasi ya upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ilikuwa na sehemu tatu ambazo ni; A, B na C zenye jumla ya maswali saba yenye alama 100. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili (1 na 2), sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3, 4 na 5) na sehemu C ilikuwa na maswali mawili (6 na 7). Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote katika vipengele vyote.

Wanafunzi waliosajiliwa kufanya upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2020 walikuwa 89,393. Waliofanya upimaji walikuwa 82,338. Idadi hiyo ni ongezeko la wanafunzi 13,514 ikilinganishwa na wanafunzi 68,824 waliofanya upimaji wa somo hili mwaka 2019. Kati ya wanafunzi 89,393 waliofanya upimaji, wanafunzi 54,229 sawa na asilimia 65.94 walifaulu. Kati yao, wanafunzi 314 (0.38%) walipata daraja A, 1,527 (1.86%) walipata daraja B, 16,334 (19.86%) walipata daraja C na 36,054 (43.84%) walipata daraja D. Wanafunzi 28,006 sawa na asilimia 34.06 walifeli kwa kupata daraja F. Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu katika somo hili kwa mwaka 2020 kilikuwa kizuri kwa asilimia 70.72. Hata hivyo, kiwango hiki kilishuka kwa asilimia 15.09 kikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 85.61 uliofikiwa mwaka 2019.

Katika taarifa hii sampuli za majibu ya wanafunzi zimeambatanishwa kwa lengo la kuonesha umahiri wa wanafunzi katika kujibu maswali. Aidha changamoto zilizowakabili wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi zimebainishwa ili ziweze kufanyiwa kazi ipasavyo. Pamoja na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi, taarifa hii imebainisha ufaulu wa wanafunzi katika mada mbalimbali zilizopimwa.

Ufaulu wa wanafunzi umegawanywa katika makundi matatu ambayo ni: vizuri, wastani na dhaifu. Ufaulu ulikuwa dhaifu kama asilimia ya wanafunzi waliofanya vizuri ni 0 hadi 29; ufaulu ulikuwa wa wastani ikiwa waliofaulu swali ni kati ya asilimia 30 hadi 64 na ufaulu ni mzuri ikiwa ni

asilimia 65 hadi 100.

Hatimae, hitimisho na mapendekezo kutokana na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umetolewa katika sehemu ya mwisho ya taarifa hii. Matokeo ya uchambuzi huu yanatarajia kutumika katika kuimarisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa wanafunzi na hatimaye kuboresha kiwango cha ufaulu katika upimaji ujao.

## 2.0 UCHAMBUZI WA KILA SWALI


### 2.1 SEHEMU A: SUNNAH, HADITHI NA TAWHIID

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (1 na 2) yenye alama kumi kila moja. Maswali yalitoka katika mada za *Sunnah na Hadithi* na *Tawhiid*. Swali la kwanza lilikuwa la kuchagua jibu sahihi kutoka katika majibu manne (A, B, C na D) na lilikuwa na vipengele 10. Swali la pili lilikuwa la kuoanisha hoja kumi zilizo katika orodha A (i - x) na maneno yaliyo katika orodha B (A - O).

#### 2.1.1 Swali la 1: Sunnah na Hadithi - Kuchagua Jibu Sahihi


Swali la 1 lilikuwa na vipengele kumi (i) - (x) vilivyotolewa katika mada ndogo za: *Maana na Umuhimu wa Hadithi*, *Uandishi wa Hadithi za Mtume* (s.a.w) na *Uchambuzi wa Hadithi za Mtume* (s.a.w). Mwanafunzi alitakiwa kuchagua jibu sahihi katika majibu manne aliyopewa (A, B, C au D) kisha kuandika herufi ya jibu hilo katika kisanduku. Kila kipengele kilikuwa na alama moja, hivyo swali hilo lilikuwa na jumla ya alama 10.

Wanafunzi 82,335 (99.9%) kati ya 82,338 (100%) walijibu swali hilo. Jumla ya wanafunzi 55,343 sawa na asilimia 67.2 walipata alama 3 hadi 6 ambazo ni alama za wastani. Wanafunzi 23,705 sawa na asilimia 28.8 walipata alama 0 hadi 2 ambazo ni alama za chini za ufaulu. Aidha, wanafunzi 3,287 (4.0%) pekee ndiyo walioweza kupata alama 7 hadi 10 ambazo ni alama za ufaulu mzuri. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 1**: *Alama za wanafunzi kwa asilimia katika swali la 1.*

Uchambuzi wa takwimu za majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri. Wanafunzi 58,630 (71.20%) walipata alama kuanzia 3 hadi 10 ambazo ni alama za kufaulu katika swali hili. Wanafunzi hao walionesha umahiri katika kubaini majibu sahihi na kuchagua herufi ya jibu husika katika vipengele vitatu hadi kumi. Aidha, wanafunzi 33 (0.01%) kati ya waliofaulu vizuri waliweza kupata alama zote 10 za swali hilo. Wanafunzi hao walionesha weledi katika mada ya Sunnah na Hadithi na waliweza kutumia vema maarifa yao kuchagua herufi za majibu sahihi katika vipengele vyote. Kielelezo namba 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuchagua herufi za majibu sahihi katika vipengele vyote kumi.


1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Sunnah inapatikana kwa kuzingatia mambo gani kati ya haya?
A Maneno, vitendo na ithibati ya Mtume (s.a.w).
B Swala tano za faradhi, Zakat, Funga pamoja na Hijja.
C Maneno ya wanazuoni na vitendo vya Maswahaba (r.a).
D Ithibati ya Mtume (s.a.w) katika vitendo vya wanazuoni.
[A]

(ii) Hadithi iliyoandikwa na Maimamu wanne wa Sunnah katika orodha ya sahihi Sitta inaitwaj
A Muttafaqun Alayh. B Rawau Shaykhan
C Rawau Sunan. D Muttafaqun Shaykhan
[C]

(iii) Miongoni mwa kazi za Hadithi ni
A kuongeza thawabu B kunogesha Sunnah
C kuhifadhi Sunnah D kuongeza Qur'an.
[C]

(iv) Kwa kutumia kigezo cha usahihi, kuna aina ngapi za Hadithi?
A Mbili B Nne
C Tatu D Tano
[B]

(v) Kwa sababu gani Mtume (s.a.w) aliwakataza Maswahaba wake kuandika Hadithi hapo mwanzo?
A Walikuwa hawajui kuandika vizuri
B Yeye mwenyewe alikuwa hai
C Alitaka watekeleze zaidi kuliko kuandika
D Alihofia watachanganya na Qur'an
[D]

(vi) Ni kwanini hitajio la kuhifadhi Hadithi kwa maandishi lilijitokeza kipindi cha Maswahaba?
A Waandishi walikuwa wengi sana.
B Maswahaba wengi sana walifariki.
C Mgogoro wa kisiasa kati ya waislamu.
D Kulikuwa na harakati nyingi za mafunzo.
[C]

(vii) Nini maana ya Tabi'ina katika Historia ya uandishi wa Hadithi?
A Waliosoma kwa Maswahaba wa Mtume (s.a.w)
B Wafuasi wa wanazuoni wa Hadithi sahihi pekee
C Watu walioishi na Maswahaba wa Mtume (s.a.w)
D Maswahaba waliohama Madinah kwenda Iraq
[A]

(viii) Hadithi inayofanana na sahihi lakini wasimulizi wake wana kasoro ya kudhibiti inapewa daraja gani kati ya hizi?
A Sahihi B Hasan
C Dhaifu D Maudhu'u
[B]

(ix) Jambo gani lilimsukuma Khalifah Umar bin Abdul-Aziz kuchukua dhima ya kuchuja Hadithi
A Aliusiwa na Mtume (s.a.w)
B Kuwepo kwa wanazuoni wengi
C Kupanuka kwa dola ya Kiislamu
D Kuwepo kwa Hadithi maudhuu
[D]

(x) Ni istilahi gani hutumika kubaini Matin moja ya Hadithi iliyosimuliwa na wapokezi wengine
A Riwaya B Mutawatir
C Isnad D Mustalah Hadithi
[A]

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 1.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila kipengele umefanyika kama ifuatavyo:

Kipengele cha (i) kilimtaka mwanafunzi kuchagua orodha ya mambo ya kuzingatia ili kupata Sunnah ya Mtume (s.a.w). Wanafunzi mahiri katika dhana ya Sunnah waliweza kuchagua jibu sahihi la kipengele hicho ambalo lilikuwa herufi A *Maneno, vitendo na ithibati ya Mtume* (s.a.w). Baadhi ya wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki walichagua herufi B *Swala tano za faradhi, Zakat, Funga pamoja na Hijja.* Uchaguzi huo umetokana na kushindwa kuelewa vema matakwa ya swali kwani ibada zilizotajwa kwenye kipotoshi B siyo njia inayotosheleza kupata Sunnah zote za Mtume (s.a.w), kwakuwa yote yaliyotajwa katika kipotoshi hicho yanaingia katika

*vitendo*. Aidha, waliochagua vipotoshi *C* na *D* walishindwa kubaini kuwa Sunnah ya Mtume (s.a.w) haipatikani kwa maneno wala vitendo vya wanazuoni.

Katika kipengele cha (ii) mwanafunzi alitakiwa kuchagua jina la Hadithi iliyoandikwa na Maimamu wanne wa Sunnah katika orodha ya Sahihi Sita. Wanafunzi waliowafahamu vema Maimamu hao waliweza kutumia maarifa yao vizuri kuchagua jibu sahihi ambalo lilikuwa herufi C *Rawau Sunan*. Aidha wanafunzi walioshindwa katika kipengele hicho baadhi yao walichagua herufi A *Muttafaqun Alayh* na wengine walichagua B *Rawau Shaykhan*. Wanafunzi hao walishindwa kutambua viwakilishi vya Rawi wengine tofauti na Imam Bukhari na Muslim. Aidha, kipotoshi D *Muttafaqun Shaykhan* ni kiwakilishi ambacho hakitumiki katika Rawi wa Hadithi, ingawa kilugha kinamaanisha Imamu Bukhari na Muslim.

Katika kipengele cha (iii) mwanafunzi alitakiwa kubaini moja ya kazi za Hadithi, ambapo wanafunzi walioelewa vema dhana ya Hadithi waliweza kuchagua kwa usahihi jibu C *kuhifadhi Sunnah.* Wanafunzi hao walikuwa mahiri katika kuzielewa kazi za Hadithi. Wanafunzi walioshindwa kipengele hiki walichagua herufi D *kuongeza Qur'an*. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa Qur'an imejitosheleza hivyo haiwezi kuongezwa na Hadithi bali kutafsiriwa kivitendo. Baadhi yao walichagua kipotoshi A *kuongeza thawabu.* Jibu hilo si sahihi kwasababu *thawabu* ni matokeo ya kutekeleza maelekezo ya Hadithi na si kazi mahususi ya Hadithi. Aidha, kipotoshi B *kunogesha Sunnah* hakikuwa sahihi kwa sababu kinapingana na malengo ya Sunnah.

Kipengele cha (iv) kiliwataka wanafunzi kubaini aina za Hadithi kwa kigezo cha usahihi. Wanafunzi waliokuwa mahiri katika tanzu za Hadithi waliweza kubaini jibu sahihi ambalo lilikuwa herufi B *Nne*. Baadhi ya wanafunzi waliokosa katika kipengele hicho walichagua herufi A *Mbili,* ambacho hakikuwa sahihi kwani kategoria hiyo inaakisi aina kuu za Hadithi kwa ujumla ambazo ni Qudsiy na Nabawiy. Aidha kipotoshi C *Tatu* kiliakisi sehemu kuu za hadithi ambazo ni Sanad, Matin na Rawi. Kipotoshi D *Tano* hakikuwa sahihi kwani kategoria hiyo haitumiki katika elimu ya Hadithi.

Katika kipengele cha (v) mwanafunzi alitakiwa kuchagua sababu moja iliyosababisha Mtume (s.a.w) kuwakataza maswahaba wake kuandika

hadithi hapo mwanzo. Wanafunzi waliofahamu vema historia ya uandishi wa Hadithi katika zama za Maswahaba waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki na kuchagua herufi D *Alihofia watachanganya na Qur'an.* Wanafunzi wengine walichagua herufi B *Yeye mwenyewe alikuwa hai*. Hoja hii haikuwa sahihi kwa wakati wa mwanzo kwasababu baadae Mtume (s.aw) aliwaruhusu kuandika wakati bado akiwa hai. Aidha, kipotoshi A *Walikuwa hawajui kuandika vizuri,* hakikuwa sahihi kwasababu walikuwepo maswahaba wengi mahiri katika kusoma na kuandika. Kipotoshi C *Alitaka watekeleze zaidi kuliko kuandika,* hakikuwa sahihi kwani wakati huo pia walikuwa wakiandika Qur'an.

Katika kipengele cha (vi) mwanafunzi alitakiwa kubaini sababu ya kuibuka kwa hitajio la kuhifadhi Hadithi kwa maaandishi katika kipindi cha maswahaba. Jibu sahihi la kipengele hiki lilikuwa C *Mgogoro wa kisiasa kati ya waislamu*. Wanafunzi weledi wa historia ya uandishi wa Hadithi waliweza kuchagua jibu hilo kwa sababu walifahamu kuwa jambo hilo lilisababisha matumizi mabaya ya Hadithi za Mtume (s.a.w) kulingana na upande wa kisiasa aliokuwa nao mtu na hatimae kuibuka Hadithi maudhuu. Aidha wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki, walichagua vipotoshi A *Waandishi walikuwa wengi sana,* B *Maswahaba wengi sana walifariki* na wengine walichagua D *Kulikuwa na harakati nyingi za mafunzo*. Uchaguzi huo ulionesha kuwa wanafunzi walichanganya matukio katika historia ya Hadithi kwa sababu hoja hizo zilichukua nafasi katika kipindi kilichofuata baada ya kipindi cha maswahaba.

Katika kipengele cha (vii) mwanafunzi alitakiwa kubaini maana ya Tabi'ina katika Historia ya uandishi wa Hadithi. Wanafunzi weledi wa historia hiyo waliweza kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki kwa kuchagua herufi A *Waliosoma kwa maswahaba wa Mtume*. Wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki wengi walichagua herufi C *Watu walioishi na maswahaba wa Mtume*, jibu ambalo si sahihi kwani kuishi na Maswahaba siyo sifa ya kuwa Tabi'in bali kusoma kutoka kwao. Aidha kipotoshi B *Wafuasi wa wanazuoni wa Hadithi sahihi pekee,* hakikuwa sahihi kwasababu Tabi'ina siyo wafuasi wa wanazuoni na D *Maswahaba waliohama Madinah kwenda Iraq* haikuwa sahihi kwasababu na hawa walikuwa ni Muhajirina.

Kipengele cha (viii) mwanafunzi alitakiwa kubaini daraja la Hadithi inayofanana na sahihi lakini wasimulizi wake wana kasoro ya kudhibiti. Wanafunzi mahiri katika uchambuzi wa Hadithi waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki na kuchagua herufi B *Hasan*. Kwa upande mwingine wanafunzi waliokosa katika kipengele hiki wengi walichagua kipotoshi C *Dhaifu* kwa kuwa imetajwa kuwa wasimulizi wa Hadithi hiyo wana kasoro ya kudhibiti. Hata hivyo, wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa udhaifu wa Hadithi ni kutokana na kasoro iliyo wazi katika Isnad. Baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi D *Maudhu'u,* ambayo si sahihi kwani hiyo ni Hadithi ya uongo ambayo haina asili kwa Mtume (s.a.w). Waliochagua kipotoshi A *Sahihi* walishindwa kuelewa kuwa Hadithi sahihi ni ile ambayo haina kasoro katika kipengele chochote.

Kipengele cha (ix) kilimtaka mwanafunzi kubaini sababu iliyomsukuma Khalifa Umar bin Abdul-Aziz kuchukuwa dhima ya kuchuja Hadithi. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa D *Kuwepo kwa Hadithi maudhuu*. Wanafunzi weledi wa Historia ya uandishi wa Hadithi walijibu kwa usahihi katika kipengele hiki kwa kuwa waliifahamu vema historia hiyo. Aidha kwa wanafunzi waliokosa, wengine walichagua herufi C *kupanuka kwa dola ya kiislamu,* wanafunzi hawa walichanganya historia ya Qur'an na Hadithi kwani sababu hiyo inatajwa katika historia ya kunakiliwa na kuhaririwa kwa Qur'an. Waliochagua kipotoshi A *Aliusiwa na Mtume (s.a.w)* haikuwa sahihi kwa sababu Khalifa huyo hakuwepo wakati wa Mtume (s.a.w). Aidha kipotoshi B *Kuwepo kwa wanazuoni wengi* nacho hakikutosha kuwa jibu sahihi kwani walikuwepo wanazuoni wengi kabla ya wakati wake na jambo hilo halikufanyika.


Kipengele cha (x) kilimtaka mwanafunzi kukumbuka istilahi inayotumika kubaini Matin moja ya Hadithi iliyosimuliwa na wapokezi wengine. Wanafunzi mahiri katika mada ya Hadithi waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi A *Riwaya.* Baadhi ya wanafunzi waliokosa, walichagua kipotoshi D *Mustalah Hadith* ambayo haikuwa sahihi kwa kuwa ni istilahi inayomaanisha sayansi ya Hadithi kwa ujumla. Wengine walichagua kipotoshi B *Mutawatir* ambayo ni istilahi inayotumika kufafanua Hadithi yenye wapokezi wengi ambao haiwezekani kukubaliana uongo. Wengine walichagua kipotoshi C *Isnad* ambayo ni istilahi inayotumika kueleza msusuru wa wapokezi katika Hadithi.

Wanafunzi 23,705 (28.79%) waliopata alama za chini (0 hadi 2) walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Sunnah na Hadithi hivyo walishindwa kuchagua majibu sahihi katika vipengele vingi vya swali. Kati yao, wanafunzi 1,569 (1.9%) walipata alama 0 baada ya kushindwa kuchagua majibu sahihi katika vipengele vyote.

### 2.1.2 Swali la 2: Tawhiid - Kuoanisha

Swali hili lilitoka katika mada za Tawhiid ambazo ni; Imani ya Kiislamu Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu na Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini. Mwanafunzi alitakiwa kuoanisha taarifa zilizokuwa orodha A (i) – (x) na maneno sahihi (A) hadi (O) kutoka orodha B, kisha kujaza herufi ya jibu sahihi katika jedwali alilopewa. Kila kipengele kilikuwa na alama 1 hivyo swali hili lilikuwa na alama 10 kwa ujumla.

Wanafunzi 82,333 (99.9%) kati ya 82,338 (100%) walijibu swali hili. Kati yao wanafunzi 59,070 sawa na asilimia 71.70 walipata alama za wastani (3 hadi 6). Wanafunzi 12,342 sawa na asilimia 15.00 walipata alama za chini (0 hadi 2). Aidha, wanafunzi 10,921 sawa na asilimia 13.30 walifaulu vizuri kwa kupata alama 7 hadi 10. Kati ya waliofaulu vizuri, wanafunzi 1,085 ambao ni sawa na asilimia 1.3 waliweza kupata alama zote 10 za swali hili. Chati namba 2.1 inaonesha ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 2**: *Alama za wanafunzi kwa asilimia katika swali la 2.*

Uchambuzi wa takwimu za majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Kwa kuwa wanafunzi 69,991 (85.00%) waliojibu swali hili walipata alama 3 hadi 10 ambazo ni alama za kufaulu. Wanafunzi hawa walikuwa mahiri katika kubaini majibu sahihi na kuchagua herufi zake katika vipengele kati ya vitatu hadi kumi.

Aidha, wanafunzi 193 (0.2%) kati ya waliofaulu vizuri waliweza kupata alama zote 10 za swali hilo. Wanafunzi hao walionesha kuelewa vizuri mada za Tawhiid na waliweza kutumia vema maarifa yao kuoanisha taarifa zote na maneno sahihi. Kielelezo namba 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuoanisha vipengele vyote kwa usahihi.

2. Oanisha sentensi kutoka **Orodha A** na maneno kutoka **Orodha B** kisha jaza herufi yake katika jedwali ulilopewa.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Takrima ya kwanza aliyokirimiwa mwanadamu na Mola wake. | A Muislamu |
| (ii) Asili au chanzo cha fani zote za elimu anazozijua mwanadamu na kuzitumia hapa duniani. | B Tawhiid |
| | C Uislamu |
| (iii) Malaika aliyehusika kupeleka ujumbe kwa Mitume wa Allah (s.w). | D Al-Islam |
| (iv) Elimu ya maarifa ya Uislamu inayomfanya mtu kumtambua Mola wake na kumuabudu ipasavyo. | E Rububiyyah |
| | F Akili |
| (v) Watu ambao wanainasibisha dini na imani ya kuwepo kwa Mungu muumba. | G Allah (s.w) |
| (vi) Mfumo wa maisha unaogusa nyanja zote muhimu za binaadamu kwa mujibu wa maumbile yake. | H Washirikina |
| | I Faradh Ain |
| (vii) Mwenendo mwema wa kujisalimisha kikamilifu na kutii mamlaka ya Mwenyezi Mungu (s.w). | J Makafiri |
| (viii) Mtu anayeishi kwa kumtii Allah (s.w) na kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake. | K Shirk |
| | L Elimu |
| (ix) Imani kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja ambaye hana mshirika. | M Faradh kifaya |
| (x) Vitendo ambavyo vinakiuka itikadi ya umoja wa Mwenyezi Mungu (s.w). | N Jibril |
| | O Swala |

**Majibu**

| Orodha A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Orodha B | L | G | N | I | J | C | D | A | B | H |

Kielelezo 2.1: Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 2.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila kipengele umefanyika kama ifuatavyo;

Katika kipengele cha (i) mwanafunzi alitakiwa kubaini Takrima ya kwanza aliyokirimiwa mwanadamu na Mola wake. Wanafunzi mahiri katika Tawhiid na Historia walielewa vema matakwa ya kipengele hiki na kuchagua herufi ya jibu sahihi ambayo ni L *Elimu*. Wanafunzi waliokosa kipengele hiki wengi walichagua herufi C *Uislamu.* Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa Uislamu ni jambo ambalo waliumbiwa nalo (Qur'an 30:30) na kukamilishwa kimafunzo baada ya Hija ya mwisho ya Mtume (s.a.w) Qur'an (5:3).

Kipengele cha (ii) kilimtaka mwanafunzi kubaini asili au chanzo cha fani zote za elimu anazozijua mwanadamu na kuzitumia hapa duniani. Kipengele hicho kilikuwa kinajibiwa kwa usahihi na herufi G *Allah* (s.w). Wanafunzi waliochagua herufi G walionesha kufahamu vema dhana ya Elimu katika mtazamo wa Uislamu, hivyo waliweza kubaini jibu hilo. Aidha, wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki wengi walichagua herufi F *Akili.* Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa kuwa akili ni tegemezi katika milango ya fahamu ambayo ni dhaifu kiasili. Pia, akili ni tegemezi kwa mazingira ambayo ni tofauti baina ya jamii moja na nyingine, hivyo haiwezi kuwa chanzo.

Katika kipengele cha (iii) mwanafunzi alitakiwa kubainisha Malaika aliyehusika kupeleka ujumbe kwa Mitume wa Allah (s.w). Wanafunzi mahiri katika dhana ya kuamini Malaika walifahamu jibu sahihi la kipengele hiki na kuchagua herufi N *Jibril*. Miongoni mwa wanafunzi waliokosa kipengele hiki ni wale waliochagua kipotoshi E *Rububiyyah.* Wanafunzi hawa walishindwa kubaini kuwa *Rububiyyah* ni aina mojawapo ya Tawhiid inayohusu upweke wa Mwenyezi Mungu katika ulezi. Wengine walichagua kipotoshi I *Faradh Ain* ambacho pia hakikuwa sahihi kwani *Faradh Ain* ni jambo la lazima kwa kila mtu binafsi kulitekeleza*,* hivyo halikuwa jina la Malaika kama ambavyo swali liliuliza.

Katika kipengele cha (iv) mwanafunzi alipaswa kutambua nafasi ya Elimu ya maarifa ya Uislamu inayomfanya mtu kumtambua Mola wake na kumuabudu ipasavyo. Wanafunzi mahiri katika dhana ya Elimu katika Uislamu waliweza kutambua jibu sahihi na kuchagua herufi I *Faradh Ain*, kwakuwa jambo hilo ni lazima kwa kila mtu binafsi. Aidha, baadhi ya wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki walichagua herufi B *Tawhiid* na wengine E *Rububiyyah.* Wanafunzi hawa hawakuelewa kuwa zote mbili ni fani za *maarifa ya Uislamu* zinazohusu itikadi ya umoja Mwenyezi Mungu (s.w).

Kipengele cha (v) kilimtaka mwanafunzi kubaini watu ambao wanainasibisha dini na imani ya kuwepo kwa Mungu muumba. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa herufi J *Makafiri.* Wanafunzi waliokuwa na uelewa wa dhana ya Dini katika Uislamu waliweza kubaini jibu hilo kwa sababu walielewa maana ya neno kuinasibisha kama ilivyotumika katika sentensi ulizi. Aidha, jamii hiyo (Makafiri) ndiyo inayodai kuwa hawana Dini kwakuwa hawaamini kama kuna Mungu. Wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki, wengi walichagua herufi A *Muislamu*. Wanafunzi hawa walishindwa kujua kwamba katika Uislamu, Dini imefafanuliwa kama *Mfumo wowote wa maisha ya mwanadamu* na si *Imani ya kuwepo kwa Mungu muumba* (Qur'an 3:85) na dhana ya Mungu katika Uislamu haifungamani na *uumbaji* (Qur'an 9:31).

Kipengele cha (vi) kiliuliza kuhusu Mfumo wa maisha unaogusa nyanja zote muhimu za binadamu kwa mujibu wa maumbile yake. Wanafunzi weledi wa dhana ya Dini kwa mtazamo wa Uislamu waliweza kubaini jibu sahihi katika kipengele hiki na kuchagua herufi C *Uislamu*. Jibu hilo lilifafanua maana mahususi ya Uislamu kama Dini. Aidha, baadhi ya wanafunzi walioanisha kipengele hiki na herufi N *Jibril* ambalo ni jina la Malaika kiongozi. Wengine walichagua herufi D *Al-Islam* jibu ambalo halikutosha kuwa sahihi kwa muhtadha wa swali hilo.

Kipengele cha (vii) kiliuliza kuhusu Mwenendo mwema wa kujisalimisha kikamilifu na kutii mamlaka ya Mwenyezi Mungu. Wanafunzi mahiri katika dhana ya Dini waliweza kubaini jibu sahihi katika kipengele hiki na kuchagua herufi D *Al-Islam.* Jibu hilo lilikuwa sahihi kwa kuwa kipengele hicho kimefafanua maana mahususi ya kilugha ya neno hilo. Baadhi ya wanafunzi waliokosa kipengele hiki walichagua kipotoshi M *Faradhi kifaya.* Wanafunzi hawa walishindwa kubaini kuwa, *Faradhi kifaya* ni

lazima kwa watu wachache kwa niaba ya wengine wakati kujisalimisha na kutii mamlaka ya Mwenyezi Mungu ni jambo la lazima kwa kila mtu.

Kipengele cha (viii) kiliuliza kuhusu mtu anayeishi kwa kumtii Allah (s.w) na kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake. Wanafunzi walioifahamu vema dhana ya Uislamu kama mfumo wa maisha, waliweza kubaini jibu sahihi la kipengele hiki na kuchagua herufi A *Muislamu.* Aidha, wanafunzi waliokosa kipengele hiki walichagua herufi H *Washirikina.* Wanafunzi hawa walishindwa kubaini kuwa washirikina humshirikisha Mwenyezi Mungu (s.w) katika itikadi na ibada zao. Wengine walichagua herufi D *Al-Islam.* Wanafunzi hao walishindwa kubaini kuwa *Al-Islam* ni mfumo na siyo mtu.

Kipengele cha (ix) kiliuliza kuhusu imani kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja na hana mshirika. Kipengele hiki kilijibiwa kwa usahihi na herufi B *Tawhiid.* Aidha wanafunzi walioelewa vema imani ya Kiislamu waliweza kutambua jibu hilo na kulichagua, kwakuwa maelezo ya kipengele hiki yalitoa maana mahususi ya neno *Tawhiid* kama msingi wa itikadi ya Uislamu. Aidha, wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki baadhi yao walichagua herufi L *Elimu.* Wanafunzi hawa walishindwa kufahamu kuwa elimu siyo imani bali ni maarifa juu ya jambo fulani. Wengine walichagua herufi E *Rububiyyah* ambayo ni *Upweke au umoja wa Mwenyezi Mungu katika ulezi.* Jibu hili halikuwa sahihi kwasababu lilifafanua upande mmoja tu wa imani uliyoelezwa kwenye hoja ya swali.

Kipengele cha (x) kilimtaka mwanafunzi kubaini vitendo ambavyo vinakiuka itikadi ya umoja wa Mwenyezi Mungu (s.w). Wanafunzi waliokuwa na maarifa katika imani ya Kiislamu waliweza kutambua jibu sahihi na kuchagua herufi K *Shirk*. Aidha, baadhi ya wanafunzi waliokosa kipengele hiki walichagua herufi J *Makafiri* na wengine walichagua herufi H *Washirikina* Majibu yote mawili hayakuwa sahihi kwa sababu yalielekea makundi ya watu au jamii zilizo na itikadi kinyume na ile ya umoja wa Mwenyezi Mungu na sio vitendo kama sentensi ya swali ilivyotaka.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 12,342 (15%) kati ya waliofanya swali hili walipata alama za chini (0 hadi 2). Wanafunzi hawa walishindwa kubaini matakwa ya vipengele vingi vya swali na hatimaye kushindwa kuoanisha kwa usahihi. Wengine walichanganya dhana zilizo kinyume kama vile *Tawhiid* na *Shirk,* hivyo walichagua *Tawhiid* mahali

palipostahiki *Shirk* na kinyume chake. Wengine walichanganya *Muislamu* na *Washirikina* hivyo kuchagua *Washirikina* sehemu iliyostahiki *Muislamu*. Kwa ujumla walikosa maarifa ya kutosha katika mada za Tawhiid.

Aidha, wanafunzi 1,08 (1.3%) walipata alama 0 baada ya kushindwa kuoanisha katika vipengele vyote. Kielelezo namba 2.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuoanisha kwa usahihi katika vipengele vyote 10 vya swali.

2. Oanisha sentensi kutoka **Orodha A** na maneno kutoka **Orodha B** kisha jaza herufi yake katika jedwali ulilopewa.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Takrima ya kwanza aliyokirimiwa mwanadamu na Mola wake. | A Muislamu |
| (ii) Asili au chanzo cha fani zote za elimu anazozijua mwanadamu na kuzitumia hapa duniani. | B Tawhiid |
| | C Uislamu |
| (iii) Malaika aliyehusika kupeleka ujumbe kwa Mitume wa Allah (s.w). | D Al-Islam |
| (iv) Elimu ya maarifa ya Uislamu inayomfanya mtu kumtambua Mola wake na kumuabudu ipasavyo. | E Rububiyyah |
| | F Akili |
| (v) Watu ambao wanainasibisha dini na imani ya kuwepo kwa Mungu muumba. | G Allah (s.w) |
| (vi) Mfumo wa maisha unaogusa nyanja zote muhimu za binaadamu kwa mujibu wa maumbile yake. | H Washirikina |
| | I Faradh Ain |
| (vii) Mwenendo mwema wa kujisalimisha kikamilifu na kutii mamlaka ya Mwenyezi Mungu (s.w). | J Makafiri |
| (viii) Mtu anayeishi kwa kumtii Allah (s.w) na kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake. | K Shirk |
| | L Elimu |
| (ix) Imani kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja ambaye hana mshirika. | M Faradh kifaya |
| (x) Vitendo ambavyo vinakiuka itikadi ya umoja wa Mwenyezi Mungu (s.w). | N Jibril |
| | O Swala |

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | C | F | E | O | A | N | M | H | L | J |

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 2.


## 2.2 SEHEMU B: TAWHID, TAREKH NA QUR'AN

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3, 4 na 5) yenye jumla ya alama 40. Mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote. Swali la tatu (3) lilikuwa na vipengele kumi (i – x) ambapo mwanafunzi alitakiwa kujibu Kweli au Si kweli. Swali la nne (4) lilimtaka mwanafunzi kujaza nafasi zilizowazi kwa kuchagua maneno sahihi aliyopewa katika jedwali. Swali la tano (5) lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b) vilivyomtaka mwanafunzi kupanga nukuu alizopewa katika mpangilio sahihi.

### 2.2.1 Swali la 3: Tawhiid - Kweli au Si Kweli

Swali lilimtaka mwanafunzi kuandika "Kweli" kama sentensi aliyopewa ni Sahihi au "Si Kweli" kama sentensi si sahihi. Swali lilikuwa na vipengele 10 (i - x). Kila kipengele kilikuwa na alama moja (1). Hivyo swali lote lilikuwa na jumla ya alama kumi (10). Kipengele cha (i), (ii), (vi), (vii), (viii), (ix) na (x) vilihusu mada ya *Imani ya Kiislamu*, na kipengele cha (iii), (iv) na (v) vilihusu mada ya *Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu.*

Wanafunzi wote 82,338 (100%) waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Kati yao wanafunzi 44,078 (53.5%) walifanya vizuri na kupata alama 7 hadi 10. Wanafunzi 37,741 (45.8%) walipata alama za wastani (3 hadi 6) na wanafunzi 519 (0.6%) walipata alama za chini (0 hadi 2). Aidha, kati ya waliofanya vizuri, wanafunzi 491 (0.6%) walipata alama zote kumi za swali hili. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 3:** *Alama za wanafunzi kwa asilimia katika swali la 3*

Takwimu zinaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu katika swali hili kwa ujumla kilikuwa kizuri sana. Wanafunzi 81,819 (99.37%) ya wanafunzi wote waliojibu swali hili walipata alama kati ya 3 hadi 10 ambazo ni alama za kufaulu katika swali hili. Kati yao, wanafunzi 44,078 (53.5%) walipata alama za juu (7 hadi 10) kwani waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vingi vya swali hili. Jambo hilo lilionesha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada za Tawhiid.

Aidha, wanafunzi 491 (0.6%) walipata alama zote 10 katika swali hili. Wanafunzi hawa walionesha kuwa mahiri katika mada zote za Tawhiid na waliweza kutumia maarifa yao vema kujibu vipengele vyote kwa usahihi. Kielelezo Namba 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote kwa usahihi.

3. Andika **KWELI** kama sentensi ni sahihi au **SI KWELI** ikiwa sentensi si sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Mtu hawi Muumini kwa kudai tu, bali atakapothibitisha imani yake kwa vitendo ..KWELI..........................

(ii) Nguzo za Ihsan ni sita na zile za Imani ni tano...SI KWELI..........................

(iii) Ilham ni njia aliyoitumia Allah (s.w) kuwaelimisha Mitume tu ...SI KWELI..........................

(iv) Njia ya kwanza ya kumjua Mwenyezi Mungu ipo katika maumbile ya wanadamu wenyewe ...KWELI..........................

(v) Kwa Muislamu elimu za fani mbalimbali na akili ni vikwazo katika imani yake ..SI KWELI...

(vi) Haiwezekani kutumia sayansi kuthibitisha kuwa kuna siku ya malipo ..KWELI..................

(vii) Kuamini Qadar ni kukubali kuwa kheri zote zinatoka kwa Allah (s.w) na shari zote zinatokana na shetani ...SI KWELI..........................

(viii) Sifa zote za Mwenyezi Mungu (s.w) zimetajwa katika majina yake tisini na tisa.SI KWELI.......

(ix) Malaika ni viumbe wa Mwenyezi Mungu (s.w) walioumbwa kutokana na nuru...KWELI......

(x) Malaika wamewahi kuonekana kwa watu katika maumbile ya kibinadamu...KWELI..........

Kielelezo Na. 3.1 Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 10.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila kipengele umefanyika kama ifuatavyo:

Kipengele cha (i) kilikuwa na hoja kuwa Mtu hawi Muumini kwa kudai tu, bali atakapothibitisha imani yake kwa vitendo. Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha katika dhana ya imani kwa mujibu wa Uislamu walikubali hoja hii na kuandika jibu sahihi ambalo ni *Kweli.* Wanafunzi hawa walibaini kuwa hoja hiyo inakubaliana na mafundisho sahihi ya itikadi ya Uislamu. Wanafunzi waliokosa katika kipengele hiki, walipinga hoja hiyo na kujibu kuwa *Si Kweli.* Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa kipimo cha uumini katika Uislamu ni *A'mal* ambayo ni vitendo vya mja.

Kipengele cha (ii) kilikuwa na hoja kuwa, Nguzo za Ihsan ni sita na zile za Imani ni tano. Wanafunzi waliojua misingi ya Uislamu walipinga hoja hiyo na kujibu kwa usahihi kuwa *Si Kweli.* Wanafunzi hawa walitambua kuwa hoja hiyo inapingana na mafundisho sahihi ya Mtume (s.a.w) yanayoeleza dhana ya Ihsan na nguzo za Imani. Aidha, waliokubali hoja hii na kujibu kuwa ni *Kweli,* walikosa maarifa kuhusu misingi ya Imani na Ihsan. Nguzo ya Ihsani ni moja tu nayo ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kama vile unamuona na hata kama haumuoni basi ujue wazi kuwa Yeye anakuona. Wakati nguzo za Imani ni sita ambazo ni kumuamini Mwenyezi Mungu, Kuamini Malaika wake, kuamini vitabu vyake, Kuamini mitume wake, kuamini siku ya mwisho na kuamini Qadar yake.

Kipengele cha (iii) kilikuwa na hoja kuwa Ilham ni njia aliyoitumia Allah (s.w) kuwaelimisha Mitume tu. Jibu sahihi la hoja hii lilikuwa *Si kweli.* Wanafunzi mahiri katika mada ya Elimu kwa mtazamo wa Uislamu walijibu hoja hiyo kwa usahihi. Wanafunzi hawa walifahamu kuwa, Ilham ni njia ya kupata elimu au maarifa bila ya kujifunza katika mifumo ya kawaida au kuona mfano wake. Jambo ambalo hadi sasa linatokea kwa watu. Aidha, wanafunzi waliokubali hoja hii na kujibu kuwa ni *Kweli* walishindwa kuielewa vizuri njia ya *Ilham* na kuitafsiri dhana hiyo kama njia mahususi kwa Mitume pekee. Jambo hilo halikuwa sahihi, kwani Mwenyezi Mungu ametumia njia hiyo kutoa maarifa au ujuzi wa fani mbalimbali kwa watu wengine pia ambao siyo Mitume na Manabii.

Kipengele cha (iv) kilikuwa na hoja kuwa njia ya kwanza ya kumjua Mwenyezi Mungu ipo katika maumbile ya wanadamu wenyewe. Wanafunzi walioelewa vizuri njia za kumjua Mwenyezi Mungu, walikubaliana na hoja hiyo na kujibu kwa usahihi kuwa ni *Kweli.* Wanafunzi hawa walielewa mafundisho ya Uislamu kwamba wanadamu wote wamezaliwa na hisia za kimaumbile zinazowawezesha kubaini uwepo wa Mwenyezi Mungu zinazojulikana kama *Fitrah*. Hisia hizo zinaweza kukua au kutoweka kutokana na mazingira na malezi ya mtu. Wanafunzi waliopinga hoja hii na kujibu kuwa *Si Kweli* walikosa maarifa kuhusu dhana ya *Fitrah* na wengine walishindwa kutafsiri vema hoja iliyotolewa.

Katika kipengele cha (v) kilikuwa na hoja kuwa elimu za fani mbalimbali na akili ni vikwazo katika imani ya Muislamu; Wanafunzi waliokuwa na maarifa katika mada ya Elimu na imani katika Uislamu walipinga hoja hii na kujibu kwa usahihi kuwa *Si kweli*. Wanafunzi hawa walielewa kuwa Mwenyezi Mungu aliwapa wanadamu vipawa hivyo ili waweze kuona na kutafakari ishara zake Qur'an (3:190) na (30:21). Aidha wanafunzi waliokubali hoja hiyo na kujibu kuwa ni *Kweli,* walionesha kuathiriwa na mitazamo kuwa akili na elimu za mazingira hazina nafasi katika Dini. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa jambo hilo linapingana na mafundisho ya Qur'an na Hadithi.

Kipengele cha (vi) kilikuwa na hoja kuwa haiwezekani kutumia sayansi kuthibitisha kuwa kuna siku ya malipo. Jibu sahihi la hoja hii lilikuwa *Kweli.* Wanafunzi walioielewa vema nguzo ya tano ya imani ya Kiislamu walikubali hoja hii na kujibu kwa usahihi. Wanafunzi hao walifahamu kuwa sayansi haina vipimo vya murua, haki, uadilifu, wema, uovu, halali wala haramu. Kwa sababu hiyo, sayansi haikubaliani pia na kuwepo kwa siku ambayo wanadamu watalipwa kulingana na waliyoyafanya katika maisha yao kwa mizani ya mambo hayo yaliyotajwa. Aidha, wanafunzi waliopinga hoja hiyo na kujibu kuwa ni *Si kweli,* baadhi yao walishindwa kuelewa sentensi ulizi iliyotumika na kuchanganya dhana ya "*siku ya malipo*" na "*siku ya mwisho*" kwa sababu ni kweli kuwa sayansi inathibitisha kuwepo kwa *siku ya mwisho*.


Kipengele cha (vii) kilikuwa na hoja kuwa kuamini Qadar ni kukubali kuwa kheri zote zinatoka kwa Allah (s.w) na shari zote zinatokana na shetani. Jibu sahihi la hoja hii lilikuwa *Si Kweli.* Wanafunzi waliojibu kwa usahihi katika kipengele hiki walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya Qadar. Hivyo walifahamu kuwa msingi wa itikadi hiyo ni kukiri kuwa yote yanayomfika mwanadamu yanatoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w). Aidha, wanafunzi waliokubali hoja hiyo na kujibu kuwa ni *Kweli,* walishindwa kuelewa kuwa hakuna jambo lolote linaloweza kumpata mtu bila ya idhini ya Mwenyezi Mungu (s.w).

Kipengele cha (viii) kilikuwa na hoja kwamba sifa zote za Mwenyezi Mungu (s.w) zimetajwa katika majina yake tisini na tisa. Wanafunzi walioelewa vema nguzo ya kwanza ya imani ya Kiislamu walipinga hoja hiyo na kujibu kwa usahihi kuwa *Si Kweli.* Wanafunzi hawa walifahamu kwamba hoja hiyo inapingana na Qur'an (18:109) na (31:27). Katika aya hizo Mwenyezi Mungu ametoa mifano kuwa, kama bahari zingekuwa wino na miti yote kuwa kalamu ili kuandika uwezo na sifa zake, basi bahari zote zingekauka na bado zisingeweza kumaliza sifa na uwezo wake. Aidha, wanafunzi waliokubali na kujibu kuwa ni *Kweli,* walishindwa kuelewa kuwa sifa za Mwenyezi Mungu (s.w) zimeambatana na uwezo wake, na hakuna anayejua mwisho wa uwezo wake ila Yeye mwenyewe.

Kipengele cha (ix) kilikuwa na hoja kuwa Malaika ni viumbe wa Mwenyezi Mungu (s.w) walioumbwa kutokana na nuru. Jibu sahihi la kipengele hiki lilikuwa ni *Kweli.* Wanafunzi waliojibu kwa usahihi katika kipengele hiki walionesha kufahamu vema nguzo ya pili ya imani ya Kiislamu ambayo inafafanua asili ya maumbile ya Malaika. Aidha, wanafunzi waliopinga hoja hiyo na kujibu kuwa *Si Kweli* walionesha kukosa maarifa katika nguzo ya pili ya imani ya Kiislamu hivyo kushindwa kujua asili ya maumbile ya Malaika.

Kipengele cha (x) kilikuwa na hoja kuwa, Malaika wamewahi kuonekana kwa watu katika maumbile ya kibinadamu. Wanafunzi waliokuwa na maarifa kuhusu historia ya misingi ya Uislamu na Qur'an walikubali hoja hiyo na kujibu kwa usahihi kuwa ni *Kweli.* Wanafunzi hao walifahamu kuwa upo ushahidi wa kihistoria katika Qur'an na Hadithi unaothibitisha hoja hiyo. Aidha wanafunzi waliopinga hoja hiyo na kujibu kuwa *Si Kweli,* walikosa maarifa ya kutosha kuhusu historia ya misingi ya Uislamu na Qur'an kwa ujumla.

Aidha, wanafunzi 57(0.1%) kati ya waliofanya swali hili, walipata alama 0. Baadhi yao waliacha kujibu swali na wengine walishindwa kufuata maelekezo ya swali. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kufuata maelekezo ya swali na hatimae kupata alama 0.



3. Andika **KWELI** kama sentensi ni sahihi au **SI KWELI** ikiwa sentensi si sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Mtu hawi Muumini kwa kudai tu, bali atakapothibitisha imani yake kwa vitendo Si kweli au kweli

(ii) Nguzo za Ihsan ni sita na zile za Imani ni tano. Kweli au Si kweli

(iii) Ilham ni njia aliyoitumia Allah (s.w) kuwaelimisha Mitume tu Kweli au Si kweli

(iv) Njia ya kwanza ya kumjua Mwenyezi Mungu ipo katika maumbile ya wanadamu wenyewe Kweli au Si kweli

(v) Kwa Muislamu elimu za fani mbalimbali na akili ni vikwazo katika imani yake Kweli au Si kweli

(vi) Haiwezekani kutumia sayansi kuthibitisha kuwa kuna siku ya malipo Si kweli au kweli

(vii) Kuamini Qadar ni kukubali kuwa kheri zote zinatoka kwa Allah (s.w) na shari zote zinatokana na shetani Si kweli au kweli

(viii) Sifa zote za Mwenyezi Mungu (s.w) zimetajwa katika majina yake tisini na tisa Kweli au Si kweli

(ix) Malaika ni viumbe wa Mwenyezi Mungu (s.w) walioumbwa kutokana na nuru. Si kweli au kweli

(x) Malaika wamewahi kuonekana kwa watu katika maumbile ya kibinadamu. Kweli au Si kweli


Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

Katika kielelezo Na. 3.2, mwanafunzi hakufuata maelekezo ya kujibu swali hili yaliyomtaka kuandika Kweli katika sentensi sahihi au Si kweli katika sentensi isiyo sahihi. Badala yake, aliandika *Kweli au Si Kweli* katika sentensi zote na hatimae alipata alama 0.

### 2.2.2 Swali la 4: Tarekh - Kujaza Nafasi Zilizowazi

Swali hili lilikuwa na vipengele kumi (a) hadi (j) kutoka katika mada za *Historia ya mitume walioteuliwa* na *Dhana juu ya Historia*. Swali lilimtaka mwanafunzi kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika kila kipengele kwa kutumia maneno sahihi aliyopewa kwenye kisanduku. Kila kipengele kilikuwa na alama 2 hivyo swali lote kwa ujumla lilikuwa na alama 20.

Wanafunzi 82,337 (99.9%) kati ya 82,338 (100%) waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Kati ya hao wanafunzi 60,021 (72.9%) walipata alama za wastani (5 hadi 12). Wanafunzi 13,009 (15.8%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20 na wanafunzi 9,307 (11.3%) walipata alama za chini (0 hadi 4). Aidha, wanafunzi 443 (0.5%) kati ya waliofaulu vizuri walipata alama zote 20 za swali hili. Chati Namba 4 inaonesha takwimu za ufaulu wa wanafunzi hao katika asilimia.




**Chati Na. 4**: *Alama za wanafunzi kwa asilimia katika swali la 4*

Uchambuzi wa takwimu za majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kilikuwa kizuri. Wanafunzi 73,030 (88.70%) kati ya waliojibu walipata alama 6 hadi 20. Wanafunzi hawa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vitatu au zaidi kati ya vipengele kumi vya swali.

Wanafunzi 443 (0.5%) waliopata alama zote 20 za swali hili walionesha umahiri katika mada za Tarekh na kuelewa vema matakwa ya kila kipengele katika swali. Hivyo, waliweza kuchagua majibu sahihi katika vipengele vyote 10. Kielelezo Namba 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuchagua majibu sahihi katika vipengele vyote 10 vya swali.

4. Kwa kutumia maneno uliyopewa, chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi wazi katika vipengele (a) – (j)

| |
|---|
| Wanadamu, Hud (a.s), Dunia, Uwezo wa kujielimisha, Khalifah, Zakaria (a.s), Historia, Kufanya ibada, Chembe hai moja, Uhai, Lut (a.s), Kuwa na Umri maalum, Udongo. |

(a) Nabii Ibrahimu (a.w) aliishi wakati mmoja na Nabii ....Lut (a.s)....

(b) Kwa mujibu wa Makafiri, hali iliyojitokeza kwa bahati mbaya na hakuna mwanzilishi wala anayeiongoza ni ....Uhai....

(c) Makafiri wanadai kuwa mwanadamu ni zao la kiumbe dhalili kinachobadilika kidogo kidogo kilicho na ....Chembe hai moja....

(d) Lengo kuu la maisha ya mwanadamu hapa duniani ni ....Kufanya ibada....

(e) Sayansi ya leo inatufundisha kuwa dunia, nyota na sayari zingine zote zina sifa gani? ....Kuwa na umri maalum....

(f) Kumbukumbu za matukio yanayohusu maisha ya wanadamu katika muda uliopita ni ....Historia....

(g) Qur'an inatufundisha kuwa maumbile yote ya ardhini na mbinguni yapo kwa ajili ya kutumikia ....Wanadamu....

(h) Historia ya Uislamu inatuonesha kuwa tangu awali mwanadamu aliumbwa akiwa na ....Uwezo wa kujielimisha....

(i) Nabii wa nne baada ya Adam (a.s) katika orodha ya manabii waliotajwa ndani ya Qur'an ni ....Hud (a.s)....

(j) Kabla ya kuumbwa Nabii Adam (a.s), Allah (s.w) aliwafahamisha Malaika kuwa atamleta kiumbe hapa duniani ambaye atakuwa ....Khalifah....

Kielelezo 4.1: Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4.

Uchambuzi zaidi katika majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa, wanafunzi 60,021 (72.9%) walipata alama za wastani (6 hadi 12). Ufaulu huo ulisababishwa na kushindwa kuchagua majibu sahihi katika baadhi ya vipengele na kupata baadhi yake.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila kipengele umefanyika kama ifuatavyo;

Kipengele (a) kiliuliza kuhusu jina la Nabii ambaye aliishi wakati mmoja na Nabii Ibrahim. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Historia ya Manabii waliweza kubaini jibu sahihi katika kipengele hiki na kuandika kuwa ni *Lut* (a.s). Aidha, baadhi ya wanafunzi waliokosa kipengele hiki walichagua jina *Zakaria* (a.s). Jibu hilo halikuwa sahihi kwa kuwa *Zakaria* aliishi wakati mmoja na mwanawe Nabii Yahya (a.s) na Issa mwana wa Maryam (a.s). Wengine walichagua jina *Hud* (a.s). Jibu hili pia halikuwa sahihi kwani *Hud* (a.s) alikuwa Nabii wa pekee katika zama zake.

Katika kipengele (b) kilichokuwa na hoja kuwa kwa mujibu wa Makafiri, hali iliyojitokeza kwa bahati mbaya na hakuna mwanzilishi wala anayeiongoza ni….” Wanafunzi walioelewa vema dhana ya Historia katika Uislamu waliweza kubaini jibu sahihi la hoja hiyo ambalo lilikuwa ni *Uhai.* Wanafunzi hao walielewa kuwa sentensi ya swali ilieleza moja ya itikadi za msingi wa Ukafiri. Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walichagua neno *Dunia,* na wengine walichagua *Udongo*. Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa vema matakwa ya kipengele hicho kwani maneno "dunia" na "udongo" kimantiki hayawezi kufafanuliwa kwa neno *hali* kama lilivyotumika katika swali.

Kipengele (c) kilikuwa na hoja kuwa "Makafiri wanadai kuwa mwanadamu ni zao la kiumbe dhalili kinachobadilika kidogo kidogo kilicho na…." Jibu sahihi la hoja hiyo lilikuwa *chembe hai moja.* Wanafunzi waliokuwa na maarifa katika Historia ya chanzo cha mwanadamu waliweza kubaini jibu hilo na kuliandika kwa usahihi. Wanafunzi hawa walibaini kuwa hiyo ni moja katika itikadi za Makafiri juu ya chanzo cha binadamu. Aidha, wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki, wengi walichagua neno *Uhai.* Wanafunzi hao walishindwa kubaini kuwa jibu hilo haliunganishi historia ya chanzo cha mwanadamu kwa mujibu wa itikadi ya Makafiri. Wengine walichagua neno *Udongo.* Waliochagua kipotoshi hiki walichanganya dhana hiyo na itikadi ya Kiislamu badala ya kujibu kulingana na madai ya *Makafiri*.

Kipengele (d) mwanafunzi alitakiwa kubaini lengo kuu la maisha ya mwanadam hapa duniani. Wanafunzi walioelewa vema mada ya Historia katika Uislamu walijibu kipengele hiki kwa usahihi kuwa ni *Kufanya Ibada*. Wanafunzi hawa walielewa kuwa jambo hilo ndiyo pekee ambalo linatosheleza kueleza hali zote anazopitia mwanadamu kulingana na vipawa vyake na mazingira yanayomzunguka. Aidha, wanafunzi wengine walijibu kipengele hiki kuwa ni *Uhai.* Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa kuwa uhai ni lengo lisilopimika kwani mwisho wa uhai ni kifo jambo ambalo lipo nje ya uwezo wa mwanadamu.

Katika kipengele (e) mwanafunzi alitakiwa kubaini sifa ambazo sayansi ya leo inatufundisha kuhusu dunia, nyota na sayari zingine. Jibu sahihi la swali hilo lilikuwa ni *kuwa na umri maalum.* Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha katika historia ya kuumbwa kwa ulimwengu waliweza kuchagua jibu hilo kwa usahihi. Wanafunzi hawa walielewa kuwa, uchunguzi wa kisayansi umegundua kwamba vitu hivyo vyote vimetokea katika kipindi fulani cha wakati. Aidha, wanafunzi waliokosa katika kipengele hiki walichagua maneno *Chembe hai moja*. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa Dunia, Nyota na Sayari zingine si vitu vyenye sifa ya uhai kama ilivyo kwa wanyama na ndege. Hivyo vinakosa sifa ya kuwa na chembe hai moja.

Katika kipengele (f) mwanafunzi alitakiwa kubaini kumbukumbu za matukio yanayohusu maisha ya wanadamu katika muda uliopita. Jibu sahihi la kipengele hiki lilikuwa neno *Historia.* Aidha, wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Historia waliweza kubaini jibu hilo. Wanafunzi hawa walielewa kuwa, ufafanuzi wa swali ulibeba maana mahususi ya neno *Historia*. Wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki walichagua maneno *Kuwa na umri maalum.* Wanafunzi hao walishindwa kubaini kuwa umri maalum ni kategoria na siyo kumbukumbu.

Katika kipengele (g) mwanafunzi alitakiwa kuchagua jibu ambalo lingekamilisha sentensi kwamba, Qur'an inatufundisha kuwa maumbile yote ya ardhini na mbinguni yapo kwa ajili ya kutumikia…. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya maumbile, walielewa vema matakwa ya kipengele hiki na kujibu kwa neno *Wanadamu.*Wanafunzi hao walielewa kuwa, hilo ndiyo lengo la kuwepo kwa maumbile hayo kwa mujibu wa Qur'an (2:29), (7:10) na (45:13).

Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walichagua maneno *Kufanya Ibada.* Wanafunzi hao walishindwa kujua kuwa *kutumikia wanadamu* ndiyo njia ya kufanya ibada kwa maumbile hayo kwa mujibu wa mafundisho ya Qur'an (2:29).

Katika kipengele (h) mwanafunzi alitakiwa kuchagua maneno sahihi kukamilisha hoja iliyosema kuwa "Historia ya Uislamu inatuonesha kuwa tangu awali mwanadamu aliumbwa akiwa na……" Jibu sahihi la hoja hiyo lilikuwa ni *Uwezo wa kujielimisha.* Wanafunzi walioelewa vizuri historia ya mwanadamu tokea kuumbwa kwake waliweza kuchagua maneno hayo. Wanafunzi hawa walielewa kuwa mwanadamu alipewa uwezo wa kujielimisha ili aweze kuyadhibiti mazingira yake. Aidha, wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki walichagua neno *Udongo.* Wanafunzi hao walielewa vibaya dhana ya asili ya maumbile ya mwanadamu badala ya kufafanua uwezo wake.

Kipengele (i) mwanafunzi alitakiwa kubaini jina la Nabii wa nne baada ya Adam (a.s) katika orodha ya manabii waliotajwa ndani ya Qur'an. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa *Hud* (a.s). Wanafunzi walioelewa vizuri historia ya Manabii walijibu kipengele hiki kwa usahihi. Wanafunzi hao walizingatia vizuri orodha ya Manabii 25 waliotajwa katika Qur'an na kubaini jibu hilo. Aidha wapo waliokosa kipengele hiki. Baadhi yao walichagua jina *Zakaria* (a.s) ambalo halikuwa jibu sahihi. Kwani Zakaria ni Nabii wa 22 katika orodha hiyo. Wengine walichagua *Lut* (a.s) ambalo pia halikuwa jibu sahihi kwa kuwa Lut (a.s) ni Nabii wa 7 katika orodha hiyo.

Katika kipengele (j) mwanafunzi alitakiwa kubaini hadhi ya kiumbe ambaye Allah (s.w) aliwafahamisha Malaika kuwa atamleta hapa duniani kabla ya kuumbwa Nabii Adam (a.s). Wanafunzi walioelewa vizuri historia ya kuumbwa kwa Nabii Adam (a.s), walibaini jibu sahihi la kipengele hiki kuwa ni *Khalifah.* Wanafunzi hawa walizingatia aya katika Qur'an (2:30) inayotaja cheo au sifa za wazi za kiumbe huyo kuwa ni kKhalifa. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walichagua neno *Wanadamu.* Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa kuwa wanadamu siyo hadhi bali ni jina la matokeo au uzao wa Adam (a.s) ambae alipewa hadhi ya kuwa Khalifah.

Wanafunzi 476 (0.6%) walipata alama 0 katika swali hili. Baadhi ya wanafunzi hao walishindwa kuelewa vema matakwa ya vipengele vyote katika swali. Wengine waliacha kujibu swali hili kutokana na kutokuwa na ufahamu juu ya mada zilizoulizwa. Kielelezo Namba 4.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuchagua majibu sahihi katika vipengele vyote.

4. Kwa kutumia maneno uliyopewa, chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi wazi katika vipengele (a) – (j)

| |
|---|
| Wanadamu, Hud (a.s), Dunia, Uwezo wa kujielimisha, Khalifah, Zakaria (a.s), Historia, Kufanya ibada, Chembe hai moja, Uhai, Lut (a.s), Kuwa na Umri maalum, Udongo. |

(a) Nabii Ibrahimu (a.w) aliishi wakati mmoja na Nabii ......Zakaria......

(b) Kwa mujibu wa Makafiri, hali iliyojitokeza kwa bahati mbaya na hakuna mwanzilishi wala anayeiongoza ni ......Historia......

(c) Makafiri wanadai kuwa mwanadamu ni zao la kiumbe dhalili kinachobadilika kidogo kidogo kilicho na ......Udongo......

(d) Lengo kuu la maisha ya mwanadamu hapa duniani ni ......Uhai......

(e) Sayansi ya leo inatufundisha kuwa dunia, nyota na sayari zingine zote zina sifa gani? ......Chembe hai moja......

(f) Kumbukumbu za matukio yanayohusu maisha ya wanadamu katika muda uliopita ni ......Kuwa na umri maalumu......

(g) Qur'an inatufundisha kuwa maumbile yote ya ardhini na mbinguni yapo kwa ajili ya kutumikia ......Kufanya ibada......

(h) Historia ya Uislamu inatuonesha kuwa tangu awali mwanadamu aliumbwa akiwa na ......Udongo......

(i) Nabii wa nne baada ya Adam (a.s) katika orodha ya manabii waliotajwa ndani ya Qur'an ni ......Zakaria......


(j) Kabla ya kuumbwa Nabii Adam (a.s), Allah (s.w) aliwafahamisha Malaika kuwa atamleta kiumbe hapa duniani ambaye atakuwa ......Mwanadamu......

Kielelezo Na. 4.2; Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4.

### 2.2.3 Swali la 5: Qur'an - Kupanga Nukuu Katika Mpangilio Sahihi

Swali hili lilitoka katika mada ya Qur'an na lilikuwa na vipengele viwili; (a) na (b). Kipengele (a) kilikuwa na baadhi ya aya za *Suratul Fat-ha* na kipengele (b) kilikuwa na aya za *Suratul Falaq*. Katika kila kipengele mwanafunzi alitakiwa kupanga nukuu za aya hizo katika mtiririko sahihi ili kupata maana iliyokamilika. Kila kipengele kilikuwa na alama 5, hivyo swali lote lilikuwa na jumla ya alama 10.

Wanafunzi 82,334 (99.9%) kati ya 82,338 (100%) walijibu swali hili. Kati ya hao, wanafunzi 34,739 (42.2%) walipata alama za juu (7 hadi 10). Wanafunzi 33,778 (41.0%) walipata alama za wastani (3 hadi 6) na wanafunzi 13,817 (16.8%) walipata alama za chini (0 hadi 2). Aidha, wanafunzi 13,635 (16.6%) kati ya waliopata alama za juu walipata alama zote 10 za swali hili. Chati Namba 5 inaonesha ufaulu wa wanafunzi hao katika asilimia.




**Chati Na. 5:** *Alama za wanafunzi kwa asilimia katika swali la 5.*

Takwimu zinaonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri. Wanafunzi 68,517 (83.2%) kati ya waliojibu walipata alama 3 hadi 10. Wanafunzi hawa waliweza kupanga kwa usahihi kuanzia aya tatu hadi kumi zinazokamilisha vipengele (a) na (b). Alama za wanafunzi hawa zilitofautiana kulingana na uwezo na utambuzi wao katika kupanga kwa usahihi aya hizo.

Aidha, wanafunzi waliopata alama zote 10 katika swali hili, walionesha kuwa na ufahamu wa kutosha katika Qur'an na tafsiri. Wanafunzi hawa waliweza kufuata vizuri maelekezo ya swali na kupanga sentensi zote kama ilivyotakiwa. Kielelezo Namba 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kupanga kwa usahihi nukuu hizo katika vipengele vyote viwili.

5. Nukuu zifuatazo hazikupangwa katika mtiririko unaotakiwa. Panga nukuu hizo katika mpangilio sahihi ili kupata maana iliyokamilika. Andika namba ya sentensi katika jedwali.

(a) Katika Swala zetu tunamuomba Mwenyezi Mungu (s.w) atuongoze ili tubaki kuwa katika njia sahihi kama ifuatavyo:

(i) Sio ya wale waliokasirikiwa, wala ya wale waliopotea

(ii) Wewe tu ndiye tunayekuabudu

(iii) Njia ya wale uliowaneemesha

(iv) Tuongoze katika njia iliyonyooka.

(v) Wewe tu ndiye tunayekuomba msaada.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| II | V | IV | III | I |

(b) Allah (s.w) ametuelekeza njia ya kujikinga dhidi ya shari mbalimbali za viumbe wake kama ifuatavyo:

(i) Na shari ya giza la usiku liingiapo.

(ii) Na shari ya hasidi anapohusudu.

(iii) Sema Najikinga kwa Mola wa ulimwengu wote.

(iv) Na shari ya wale wanaopuliza mafundoni.

(v) Na shari ya alivyoviumba.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| III | V | I | IV | II |

Kielelezo 5.1 Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 5

Wanafunzi 33,778 (41.00%) waliopata alama za wastani (3 hadi 6) waliweza kupanga kwa usahihi baadhi ya aya na kukosea aya zingine. Wanafunzi hao walichanganya nafasi za aya hizo kulingana na mpangilio wa Qur'an hivyo walipata alama za wastani.

Wanafunzi 13,817 (16.80%) walipata alama za chini 0 hadi 2. Wanafunzi hawa walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Qur'an, hususani tafsiri ya sura zilizochaguliwa. Baadhi ya wanafunzi hao walishindwa kujibu vipengele vyote viwili na wengine walishindwa kufuata maelekezo ya swali. Wengine walikosa kwa sababu ya kuandika majibu yao kwa herufi za kiarabu. Aidha, wanafunzi wengine walinukuu aya hizo katika sehemu za kujibia na wengine waliacha kujibu swali hili katika vipengele vyote viwili. Kielelezo Namba 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kupanga nukuu hizo kwa usahihi katika vipengele vyote viwili.

5 Nukuu zifuatazo hazikupangwa katika mtiririko unaotakiwa. Panga nukuu hizo katika mpangilio sahihi ili kupata maana iliyokamilika. Andika namba ya sentensi katika jedwali.

(a) Katika Swala zetu tunamuomba Mwenyezi Mungu (s.w) atuongoze ili tubaki kuwa katika njia sahihi kama ifuatavyo:

(i) Sio ya wale waliokasirikiwa, wala ya wale waliopotea

(ii) Wewe tu ndiye tunayekuabudu

(iii) Njia ya wale uliowaneemesha

(iv) Tuongoze katika njia iliyonyooka.

(v) Wewe tu ndiye tunayekuomba msaada.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| iv | ii | v | i | iii |

(b) Allah (s.w) ametuelekeza njia ya kujikinga dhidi ya shari mbalimbali za viumbe wake kama ifuatavyo:

(i) Na shari ya giza la usiku liingiapo.

(ii) Na shari ya hasidi anapohusudu.

(iii) Sema Najikinga kwa Mola wa ulimwengu wote.

(iv) Na shari ya wale wanaopuliza mafundoni.

(v) Na shari ya alivyoviumba.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| v | iii | iv | ii | i |

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.


### 2.3 SEHEMU C: FIQH

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (6 na 7) ambapo kila moja lilikuwa na alama 20 na kufanya jumla ya alama 40. Maswali yote mawili yalitoka katika mada za Fiqh. Mwanafunzi alitakiwa kujibu kwa ufupi katika swali la sita (6) na kujibu kwa muundo wa insha katika swali la saba (7).

#### 2.3.1 Swali la 6: Kujibu kwa Ufupi


Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (a) hadi (e) kutoka katika mada ndogo za *Kusimamisha Swala*, *Shahada*, *Kumswalia maiti* na *Chimbuko la Fiqh*. Mwanafunzi alitakiwa aidha atofautishe dhana alizopewa au atoe hoja au ataje sababu na kufafanua kwa ufupi baadhi ya dhana. Kila kipengele katika swali hili kilikuwa na alama 4 hivyo swali lote lilikuwa na alama 20.

Wanafunzi 82,294 (99.9%) kati ya 82,338 (100%) walijibu swali hili. Kati yao wanafunzi 73,968 (89.8%) walipata alama za chini (0 hadi 5.5). Wanafunzi 8,101 (9.8%) walipata alama za wastani (6 hadi 12.5) na wanafunzi 325 (0.39%) walifanya vizuri na kupata alama 13 hadi 18.5 kati ya alama 20 za swali hilo. Aidha, wanafunzi 23,753 (28.9%) walipata alama 0. Chati Namba 6 inaonesha ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na 6:** *Alama za wanafunzi kwa asilimia katika swali la 5.*

Takwimu za majibu ya wanafunzi zinaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa dhaifu. Wanafunzi 73,868 (89.8%) kati ya 82,294 (99.9%) waliofanya swali hili walipata alama za chini (0 hadi 5.5). Miongoni mwao wanafunzi 23,753 (28.9%) walipata alama 0. Wanafunzi hawa walishindwa kujibu vipengele vyote vya swali kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada za Fiqh na wengine walishindwa kujenga hoja na kuiwasilisha kwa ufasaha. Aidha, baadhi ya wanafunzi waliacha kujibu vipengele vyote vya swali. Kielelezo Namba 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika vipengele vyote vitano vya swali.


6. Jibu maswali yote (a) – (e) kwa ufupi.

(a) Tofoutisha Swala za Sunnah na Sunnah za Swala.

(b) Kwa nini Shahada haikamiliki bila ya kumshuhudia Mtume (s.a.w)?

(c) Taja sababu mbili za kutamka Shahada mbele ya Muislamu au kundi la Waislamu wakati wa kusilimu.

(i)

(ii)

(d) Bainisha kinachosomwa na mtu anayemswalia maiti katika hatua zifuatazo:

(i) Baada ya kutia nia na kuleta Takbira ya kwanza.

(ii) Baada ya Takbira ya pili.

(iii) Baada ya Takbira ya tatu.

(iv) Baada ya Takbira ya nne

(e) (i) Nini maana ya Fiqh-Ibadat?

(ii) Nini maana ya Fiqh-Muamalat?

Kielelezo Na 6.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 6.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi katika kila kipengele umefanyika kama ifuatavyo;

Katika kipengele (a) mwanafunzi alitakiwa kutofautisha Swala za Sunnah na Sunnah za Swala. Wanafunzi waliokuwa na maarifa katika Fiqh ya Swala waliweza kutambua vema matakwa ya kipengele hiki na kutofautisha kwa usahihi kwa kuandika kuwa; *Swala za Sunnah ni aina za Swala ambazo zimefundishwa na Mtume (s.a.w) nje ya Swala tano za faradhi wakati Sunnah za swala ni vipengele ambavyo mwenye kuswali akivitekeleza husaidia katika kupandisha daraja la swala yake, na kuipa nguvu ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa*.

Wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki, majibu yao yalitofautiana kwa sababu mbalimbali. Baadhi yao walionesha kutoelewa matakwa ya swali na hatimae kujibu hoja ambazo hawakuulizwa. Wengine walitofautisha Swala na Sunnah badala ya Swala za Sunnah na Sunnah za Swala. Pia wapo walioeleza umuhimu wa Sunnah katika Uislamu na wengine walitofautisha Kusimamisha Swala na Kuswali. Mambo haya yote hayakuulizwa katika swali la msingi.

Wanafunzi wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha, hivyo walijibu kipengele hicho kwa kutoa hoja zinazopishana baina yake katika hukumu, kama vile: *Swala za Sunnah ni swala ambazo ukiswali utapata thawabu na usiposwali hupati dhambi lakini Sunnah za Swala ni mambo ambayo ya lazima kuyafanya katika Swala.* Majibu haya pamoja na kuwa siyo sahihi lakini pia yalitofautiana yenyewe katika hukumu.

Baadhi ya wanafunzi walijibu kuwa: *Swala za sunnah ni swala ambazo huswaliwa pale ambapo una udhu tu na Sunnah za swala huswaliwa na watu ambao hawana udhu.* Jibu hili liliashiria kuwa mwanafunzi hakuwa na maarifa kabisa kuhusu Swala, kwani hakuna Swala inayotekelezwa bila ya udhu.

Wengine walijibu kuwa; *Swala za Sunnah ni swala ambayo huswaliwa kwa rakaa mbili au zaidi na Sunnah za swala ni kuswali kabla ya kuanza swala za Ijumaa au siku yoyote ile.* Jibu ambalo pia liliashiria kutokuwa na maarifa ya kutosha katika Fiqh ya Swala.

Katika kipengele (b) mwanafunzi alitakiwa kutoa sababu inayobainisha kwa nini Shahada haikamiliki bila ya kumshuhudia Mtume (s.a.w). Wanafunzi walioelewa vizuri nguzo ya kwanza ya Uislamu waliweza kujibu hoja hiyo kwa usahihi na kueleza kuwa: *Ni lazima kumshuhudia Mtume (s.a.w) kwa sababu yeye ndiye mwalimu aliyeteuliwa na Allah* (sw) *kuja kutufundisha juu ya kuwepo kwake Yeye Mwenyezi Mungu na Jinsi ya kumuabudu ipasavyo.* Wanafunzi hawa walionesha kuelewa vema swali na kuwa na maarifa ya kutosha juu ya Shahada. Hivyo waliweza kuwasilisha hoja hiyo kwa ufupi na kwa ufasaha.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliofanya vibaya katika kipengele hiki baadhi yao, walishindwa kutambua matakwa ya swali na kutoa majibu tofauti, kama vile*; (i) Ametumwa kuendeleza uislamu ulimwenguni (ii) Mtume ndiye atayekuja kuwaombea watu wa motoni msamaha, (iii) Makafiri hawamuamini mtume (s.a.w).* Majibu haya yanaonesha wanafunzi hao walieleza sifa za Mtume (s.a.w) ambazo hazikuwa ni msingi wa swali katika kipengele hiki. Mwanafunzi mmoja alijenga hoja kuwa *bila ya kumshuhudia Mtume hawezi kukupa kile unachokitaka,* hoja ambayo haikuwa na uhusiano na Shahada. Majibu hayo yanaonesha kuwa mwanafunzi hakuelewa vema matakwa ya swali katika kipengele hiki.

Aidha, mwanafunzi mwingine alijibu kuwa: *Kwasababu tunatakiwa tumuombe na tumtukuze na tumshukuru kwa yote anayotufanyia hapa duniani na uko akhera pia.* Majibu haya yanaonesha kutofahamu nafasi ya Mtume (s.a.w) kwani maelezo hayo yaliakisi nafasi ya Mwenyezi Mungu (s.w) na si Mtume au mwingine yeyote.

Katika kipengele (c) mwanafunzi alitakiwa kutaja sababu mbili za kutamka Shahada mbele ya Muislamu au kundi la Waislamu wakati wa kusilimu. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha katika nguzo ya kwanza ya Uislamu waliweza kubainisha sababu hizo kwa usahihi kuwa ni: (i) *Ili kuweza kujulikana au kufahamika kwa ummah wa kiislamu na kupata haki zako kwa ndugu zako wapya katika Imani. (ii) Ili uweze kushirikiana na waislamu wenzako katika kukamilisha wajibu wa kusimamisha uadilifu katika jamii.* Wanafunzi hawa walielewa vema matakwa ya swali na waliweza kuwasilisha hoja zao kwa ufasaha.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walishindwa kutambua vema matakwa ya swali. Hivyo, hawakuweza kueleza sababu mahususi zinazofafanua ulazima wa kutamka Shahada mbele ya Waislamu wakati wa kusilimu. Wengi walieleza sababu za jumla au faida zinazopatikana katika tamko la Shahadah. Wanafunzi hao walieleza kuwa: *Ili kuwaaminisha waumini na waislamu kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja,* wengine waliandika; *Ili kumpwekesha Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema,* na wengine waliandika; *Ili kukumbuka kuwa Mwenyezi Mungu yupo.* Ingawa mambo hayo yaliyotajwa yanapatikana katika Shahada, lakini hayakuonesha ulazima wa kutamka kalima hiyo wakati wa kusilimu.

Kipengele (d) kilikuwa na vipengele vidogo vinne (i) hadi (iv). Mwanafunzi alitakiwa kubainisha kinachosomwa na mtu anayemswalia maiti kila baada ya Takbira. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha katika Swala ya maiti waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki na kutaja visomo vifuatavyo: (i) *Kusoma Suratul Fat-ha. (ii) Kumswalia Mtume kwa ukamilifu. (iii) Kumuombea dua maiti (iv) Kuwaombea dua waumini na kutoa salamu.* Wanafunzi hawa walielewa vema matakwa ya swali husika na kujibu vipengele vyake vyote kwa usahihi. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walitaja mambo mbalimbali yaliyotofautiana. Baadhi yao walishindwa kuelewa vema matakwa ya swali na kufananisha Swala ya maiti na Swala za Idi mbili. Watahiniwa hawa walijibu kwa kukariri Takbira kila baada ya Takbira. Mwanafunzi mmoja ambae alishindwa kuelewa matakwa ya swali hili alitaja mambo muhimu anayopaswa kufanyiwa maiti Muislamu ambayo ni: *(i) Mnamuosha (ii) Mna mvalisha sanda (iii) Mnaenda kumuombea dua (iv) Mnaenda kumzika.* Majibu haya hayakuwa sahihi kwa mnasaba wa swali, kwani swali lilitaka ufafanuzi wa namna ya kutekeleza hoja ya tatu (iii) aliyoiandika katika majibu yake.

Wanafunzi wengine walitaja mambo yafuatayo: *(i) kusimama (ii) kuanza kusoma dua (iii) kuwataka wote wanaomdai (iv) msomaji humsomea maiti dua na kwenda kumzika.* Wanafunzi hawa walionesha kuwa na uzoefu wa utekelezaji wa kivitendo kwa baadhi ya vitendo vinavyofanyika katika swala hiyo, hata hivyo hawakuwa wanafahamu kinachosomwa katika swala hiyo.

Kipengele (e) kilikuwa na vipengele vidogo viwili (i) na (ii) vilivyouliza maana ya Fiqh-Ibaadat na Fiqh-Muamalat mtawalia. Wanafunzi waliojibu kwa usahihi katika kipengele hiki walionesha kuwa mahiri katika mada ya Fiqh na waliweza kuwasilisha majibu yao kwa ufasaha na mifano anuai. Majibu yaliyotolewa na wanafunzi hao yalikuwa; *(i) Fiqh Ibaadat ni tawi la Fiqh linalohusika katika kuchambua na kutoa ufafanuzi wa ibada maalum kama vile Swala, Zakat, Funga na Hijjah (ii) Fiqh muamalat ni tawi la Fiqh linalohusika katika kufafanua mambo mbalimbali katika jamii kama vile ndoa,biashara na ujirani.*

Wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki walitofautiana majibu kwa namna mbalimbali. Mwanafunzi mmoja alieleza kuwa: *(i) Fiqh Ibaadat ni fiqh ambayo asili au chanzo cha fani zote za elimu mwanadamu huweza kuzitumia hapa duniani.* Mwanafunzi huyu alionesha kutokuwa na maarifa kuhusu Fiqh kwa ujumla kwa kuwa majibu yake yalionesha kuchanganya dhana ya Fiqh na dhana ya elimu katika Uislamu.

Wanafunzi wengine walizieleza dhana hizo kama aina za Tawhiid na kujibu kuwa: *Fiqh Ibadat ni kumpwekesha Allah* (s.w) *na Mtume wake katika Ibada.* Maelezo hayo yalifafanua dhana ya *Tawhiid Uluhiyyah* au *Tawhiid Ibada* hivyo, hayakuwa sahihi kufafanua dhana ya Fiqh Ibadat. Aidha, wengine walizifafanua dhana hizi kama aina za najisi na kujibu kuwa: (i) *Fiqhi Ibadaat ni najisi zote isipokuwa mbwa na nguruwe,* na (ii) *Fiqhi muamalat ni mkojo wa mtoto mdogo ambae ananyonya maziwa ya mama yake na mtoto huyo awe ni wa kiume.* Maelezo haya yalifafanua dhana ya *Najisi* na si aina za Fiqh kama swali lilivyouliza.


Katika kuifafanua dhana ya Fiqh Muamalat, baadhi ya wanafunzi walieleza kuwa: *Fiqh muamalat ni aina ya Fiqh inayohusiana na sunnah za mtume,* na wengine walieleza kama: *ni Fiqh ambayo inajishughulisha na wanazuoni wengi.* Majibu haya yalionesha kuwa, wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Fiqh hivyo walikuwa wakichanganya mawazo mbalimbali kutoka katika fani tofauti na kuunganisha majibu ambayo hayakuwa na uhusiano na swali.

Pamoja na majibu ya wanafunzi hawa, wapo waliofafanua dhana hiyo kama aina ya ibada, na kueleza kuwa: *Fiqh Muamalat ni aina ya ibada inayojishughulisha na matendo ya kiimani.* Mwingine alieleza kama kitabu na kuandika kuwa: *Fiqh muamalat ni kitabu ambacho kinafunza na kina*

*maarifa ya Sunnah na maelekezo ya mambo ya dini yaliyomo katika swala na dini.* Kwa ujumla majibu ya wanafunzi hawa, yanaonesha kutokuwa na maarifa kuhusu Fiqh na aina zake.

Wanafunzi 8,101 (9.84%) walipata alama za wastani (6 hadi 12.5) baadhi ya wanafunzi hawa walijibu vipengele vichache na kuacha vingine. Wengine walijibu vipengele vyote lakini hawakuweza kutoa maelezo yakutosha katika baadhi ya dhana, hivyo hawakuweza kupata alama kamili katika vipengele hivyo.

Wanafunzi 325 (0.39%) pekee ndiyo walioweza kupata alama za juu kati ya 13 hadi 18.5. Aidha, hakuna mwanafunzi aliyepata alama zote 20 katika swali. Wanafunzi waliopata alama 18.5 za swali hili walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada za Fiqh na waliweza kujibu vipengele vingi kwa ufasaha baada ya kuelewa vema matakwa ya vipengele hivyo. Kielelezo Namba 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika vipengele vingi.



6. Jibu maswali yote (a) – (c) kwa ufupi.

(a) Tofoutisha Swala za Sunnah na Sunnah za Swala.

(b) Kwa nini Shahada haikamiliki bila ya kumshuhudia Mtume (s.a.w)?

(c) Taja sababu mbili za kutamka Shahada mbele ya Muislamu au kundi la Waislamu wakati wa kusilimu.

(i)

(ii)

(d) Bainisha kinachosomwa na mtu anayemswalia maiti katika hatua zifuatazo:

(i) Baada ya kutia nia na kuleta Takbira ya kwanza.

(ii) Baada ya Takbira ya pili.

(iii) Baada ya Takbira ya tatu.

(iv) Baada ya Takbira ya nne

(e) (i) Nini maana ya Fiqh-Ibaadat?

(ii) Nini maana ya Fiqh-Muamalat?


Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo N. 6.2 mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi katika vipengele vyote isipokuwa kipengele (C) ambacho hakutoa maelezo yaliyotosheleza hivyo alishindwa kupata alama kamili. Mwanafunzi alitakiwa kueleza (i) Kutambulika na jamii ya waislamu na kupata haki zako kutoka kwa ndugu zako wapya katika imani. (ii) Uweze kushirikiana na waislamu wenzako katika kukamilisha wajibu wa kusimamisha uadilifu katika jamii.

### 2.3.2 Swali la 7: Insha

Swali hili lilitoka katika mada ya Fiqh ya Funga, ambapo mwanafunzi alitakiwa kubainisha sifa tano za Waislamu wanaolazimika kutekeleza ibada ya Funga ya Ramadhani. Swali lilikuwa la muundo wa insha lenye alama 20.

Wanafunzi 82,136 (99.8%) kati ya 82,338 (100%) walijibu swali hili. Kati yao wanafunzi 60,420 (73.6%) walipata alama za chini (0 hadi 5.5). Wanafunzi 17,452 (21.2%) walipata alama za wastani (6 hadi 12.5) na wanafunzi 4,264 (5.9%) walipata alama za juu (13 hadi 20). Aidha, wanafunzi 22,464 (27.3%) walipata alama 0. Chati namba 7 inaonesha ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.





**Chati Na 7**: *Alama za wanafunzi kwa asilimia katika swali la 7*

Uchambuzi wa takwimu za majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa chini. Wanafunzi 60,420 (73.6%) waliojibu swali hili walipata alama hafifu (0 hadi 5.5). Kati yao wanafunzi 22,464 (27.3%) walipata alama 0. Wanafunzi hawa walishindwa kubainisha sifa tano za Waislamu wanaolazimika kutekeleza ibada ya Funga ya Ramadhani kwa sabababu mbalimbali.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika swali hili umebaini kuwa, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi walishindwa kubaini matakwa ya swali hivyo kushindwa kutoa sifa zilizohitajika. Baadhi ya wanafunzi hawa walieleza nguzo tano za Uislamu badala ya sifa tano za Muislamu anayelazimika kufunga na wengine wakaeleza nguzo za Imani. Wanafunzi wengine walieleza mambo yanayosababisha kuharibu Funga kama vile: *kula na kunywa kwa makusudi, kujitapisha kwa makusudi, kujamiiana mchana wa Ramadhani na kujitoa manii kwa makusudi.* Wengine walieleza mambo ya kufanya au ya kuzingatiwa ili kuimarisha thamani ya Funga kama vile: *kusema ukweli, kujiepusha na dharau, kujiepusha na matusi na kuwa muadilifu.* Hoja hizi zinaonesha kuwa wanafunzi hawa hawakuelewa matakwa ya swali. Hivyo hawakujibu swali la msingi na hatimaye kushindwa kupata alama.

Wanafunzi wengine walijibu kuwa: Awe *ametia nia, anaswali kwa wakati, awe anampwekesha Mwenyezi Mungu, awe anatoa Zakat na Sadakat*, *awe ameridhia kutoka moyoni na awe anaficha sehemu zake za siri.* Wanafunzi hawa walijikita katika kueleza sifa nzuri za Muumini ambazo zilikuwa kinyume na matakwa ya swali. Hivyo kukosa alama katika swali hili.

Kwa ujumla, majibu ya wanafunzi hawa yanaonesha kukosa maarifa ya kutosha katika mada ya Nguzo za Uislamu hususani mada ndogo ya Funga ya Ramadhani. Kielelezo Namba 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili.



7. Bainisha sifa tano za Waislamu wanaolazimika kutekeleza ibada ya Funga ya Ramadhani.

Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Namba 7.1 mwanafunzi alishindwa kujibu swali lililomtaka aeleze sifa za Waislamu wanaolazimika kufunga mwezi wa Ramadhani. Badala yake alieleza sifa za jumla za Waislamu ambazo hazibainishi ulazima wa kufunga au kuacha kufunga.

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa, wanafunzi 17,452 (21.2%) waliopata alama za wastani katika swali hilo walichanganya katika majibu yao yaliyo sahihi na mengine yasiyo sahihi. Baadhi yao waliandika hoja sahihi za swali lakini walishindwa kutoa maelezo yanayotosheleza katika kufafanua hoja zao. Wengine waliandika hoja chache kinyume na matakwa ya swali na kusababisha kupata alama za wastani.

Aidha, wanafunzi 4,264 (5.2%) kati ya waliofanya swali hili walipata alama za juu (13 hadi 20). Wanafunzi hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Fiqh ya Funga na kutambua vema mahitaji ya swali hilo. Hivyo, waliweza kubainisha sifa sahihi za Waislamu wanaolazimika kutekeleza ibada ya Funga ya Ramadhani. Sifa walizotoa wanafunzi hawa ni pamoja na: *Wenye akili timamu, waliofikia baleghe, wenye afya, wakazi wa mji na wanawake walio twahara.* Wanafunzi 38 (0.01%) walipata alama zote 20 katika swali hili. Wanafunzi hao walibainisha sifa hizo vizuri na kufafanua majibu yao kwa ufasaha. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.



7. Bainisha sifa tano za Waislamu wanaolazimika kutekeleza ibada ya Funga ya Ramadhani.

Funga ya Ramadhani ni funga ambayo ni faradhi kwa muislamu kutekeleza pia funga inahusiana na mataala mazima ya kujizuia na kula, kunywa au matendo yote ambayo yanaweza kufunguza. Zifuatazo ni sifa za muislamu anaye lazimika kufunga

Aliye baleghe. Muislamu anaye lazimika kufunga mwezi wa Ramadhani anatakiwa awe amebaleghe yaani kufikia umri ambao anaandikiwa madhambi na swaladu pia katika kipindi hiki cha baada ya kubaleghe atakuwa na uwezo wa kumili vyema kujizuia na matendo maovu

Wenye afya. Mtu anayefunga Saumu ya Ramadhani anatakiwa awe na afya nathubuti kama tulivyo ona hapo awali kuwa funga ni hali ya kujizuia na kula pamoja na kunywa, mtu anayefunga anatakiwa kuwa na afya nzuri yenye kuhimili funga.

Wakazi wa mji. Mkaziwa wa mji pia ni miongoni ya watu wanaolazimika kufunga funga ya Ramadhani mfano muislamu kusafiri safari na ni mkazi wa sehemu ile anatakiwa kufunga funga ya mwezi wa Ramadhani.

Kwa wanawake wasio na hedhi au nifasi. Moja ya vitu vinavyo wafanya wanawake kuto tekeleza Ibada hii ya funga ni kuwa na hedhi au nifasi hivyo basi wanawake ambao hawana au hawajapatwa na hedhi au nifasi wanalazimika kufunga.

Wenye akili timam. Muislamu asiye na akili timamu hapaswi kutekeleza Ibada hii ya funga ya ramadhani kwani mtu asiye na akili timamu hato weza kutekeleza ibada zingine ambazo ni muhimu kuto kana na uwezo wake wa kufikiri ni mdogo.

Hivyo basi hizo ni baadhi ya sifa ambazo Muislamu anatakiwa kuwanazo ili aweze kutekeleza Ibada hii ya funga katika mwezi wa Ramadhani na hata katika funga zingine za Sunnah.

Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo namba 7.2. mwanafunzi aliweza kuandika insha yenye mpangilio mzuri kuanzia utangulizi ambapo alieleza maana ya Funga ya Ramadhani, kisha alibainisha sifa za Waislamu wanaolazimika kutekeleza ibada hiyo katika kiini na kumalizia na hitimisho.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Mada zilizohusika katika upimaji huu ni *Sunnah na Hadithi*, *Tawhiid*, *Tarekh, Qur'an* na *Fiqh*. Uchambuzi wa takwimu za matokeo ya wanafunzi katika mada umeonesha kiwango kizuri cha ufaulu katika mada za; *Tawhiid (92.2%), Tarekh (88.7%), Qur'an (83.2%), Sunnah na Hadithi (71.2%).* Aidha mada ambayo ilikuwa na ufaulu wa kiwango cha chini ni *Fiqh (18.4%),* ambayo ilipimwa katika swali la sita na la saba. Mada ya *Sunnah* na *Hadithi* ilipimwa katika swali la kwanza. Mada ya *Tawhiid* ilipimwa katika swali la pili na la tatu. Katika swali la 4 ilipimwa mada ya *Tarekh* na swali la tano lilipimwa katika mada ya *Qur'an*.

Wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri katika mada za *Tawhiid*, *Tarekh, Qur'an* na katika mada ya *Sunnah* na *Hadithi*. Wanafunzi hawa walifanya vizuri katika mada hizo kwa sababu walielewa vizuri matakwa ya maswali. Na walikuwa na maarifa ya kutosha yaliyowawezesha kubaini majibu sahihi.

Wanafunzi walipata alama za chini katika mada ya *Fiqh* kwa sababu mbalimbali kama vile; kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika, kutofuata maelekezo ya swali, kutojua matakwa ya maswali na wengine kushindwa kuwasilisha majibu yao katika maelezo mafupi. Wengine kushindwa kuandika insha katika swali lililohitaji kuandikwa kwa muundo huo. Muhtasari wa takwimu kwa wastani wa kila mada umeoneshwa kwenye kiambatisho ambapo rangi nyekundu inaonesha kiwango cha chini cha ufaulu na rangi ya kijani inaonesha kiwango kizuri cha ufaulu ikiambatana na namba ya maswali katika mada husika. Aidha, hapakuwepo mada iliyokuwa na ufaulu wa wastani (njano).

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu katika upimaji huu wa kidato cha pili (FTNA 2020) katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni kizuri kwa asilimia 70.72. Uchambuzi huu umeonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa ili kuboresha zaidi kiwango cha kufaulu katika upimaji unaofuata. Changamoto zilizojitokeza kwa wanafunzi katika kujibu maswali ni pamoja na; wanafunzi kutofuata maelekezo ya swali, kushindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza, kuorodhesha majibu kwa namba au herufi kwenye swali linalohitaji kujibiwa kwa muundo wa insha, pia kukosa maarifa katika mada mbalimbali hususani mada za *Fiqh*.

Ili kuinua zaidi kiwango cha kufaulu katika upimaji ujao, juhudi za ziada zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji katika mada ya Fiqh, ili kuwapa wanafunzi maarifa ya kutosha na uwezo wa kujenga hoja. Aidha wanafunzi wanatakiwa kujengewa uwezo wa kuelewa matakwa ya maswali na kuwasilisha maarifa katika namna inayostahili. Walimu wanapaswa kutumia vitabu vya kiada na ziada vya somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ili kuwapa wanafunzi maarifa stahiki na kuepuka nadharia zisizo rasmi katika somo. Ni muhimu pia kuongeza juhudi katika ufundishaji kwa vitendo na kuwashirikisha wanafunzi katika hatua zote za ujifunzaji ili kuimarisha maarifa yao hususani katika mada ya *Fiqh.*

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu watumie njia shirikishi na kuwahamasiha wanafunzi kueleza kile wanachokifahamu kabla ya kuwafundisha ili kuwajengea uwezo wa kutoa hoja.

(b) Walimu wawaongoze wanafunzi kujadili kwa vikundi na kurejea katika vitabu vya kiada ili kupata maarifa sahihi kwa kila mada.

(c) Walimu wawapime wanafunzi ili kupata tathmini bora kuhusu maarifa na umahiri wao baada ya kufundisha kila mada na kutoa mrejesho kwa wakati ili kuwaimarisha wanafunzi.

(d) Walimu wafundishe ipasavyo mada zinazohitaji vitendo na kuhimiza wanafunzi kutekeleza na kufuatilia utekelezaji huo.

**Kiambatisho**

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA

| Na. | Mada | Ufaulu wa Kila Swali | | Asilimia ya Wanafunzi waliopata wastani wa alama 30 au zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| 1 | Tawhiid | 3 | 99.4 | 92.2 | Vizuri |
| | | 2 | 85.0 | | |
| 2 | Tarekh | 4 | 88.7 | 88.7 | Vizuri |
| 3 | Qur'an | 5 | 83.2 | 83.2 | Vizuri |
| 4 | Sunnah na Hadithi | 1 | 71.2 | 71.2 | Vizuri |
| 5 | Fiqh | 7 | 26.4 | 18.3 | Dhaifu |
| | | 6 | 10.2 | | |
| **Wastani wa Jumla wa Ufaulu** | | | | **70.72** | **Vizuri** |